# DHEHEBU NI NINI?

Ikor. 4:6 – 7

> Basi ndugu, mambo hayo nimeyafanya kuwa mfano wa mimi na Apolo kwa ajili yenu, ili kwamba kwa mfano wetu mpate kujfiunza kutokupita yale yaliyoandikwa, ili mmoja wenu asijivune kwa ajili ya huyu kinyume cha mwenziwe……….

Sikiliza vile Nabii wa Mungu alivyosema kuhusu hilo:

Sasa, hatuna kitu kinyume na watu wengine ambao ni dhehebu hatuna kitu kinyume nao, lakini nataka nielezee kwa nini hatukuenda / kufungamana na dhehebu lolote.

Sasa, sisi ni kama ushirika fulani. Sisi ni ushirika, tumeandikwa hapa mahakamani kama ushirika, kundi la watu ambalo linashirikiana pamoja ili kumuabudu Kristo. Lakini hatuko kwenye madhehebu. Hakuna mtu anayekwenda kutawala juu yetu sisi. Unaona? Sisi siyo dhehebu. Sisi ni ushirika tu wa kumwabudu Mungu miongoni mwetu waaminio wa kikristo. Watu wanakuja hapa kanisani na hapa panakuwa kanisa lao la nyumbani, kama wanapenda kuja siku zote ili mradi wanaishi. [1]

Sasa, mara imesemekana kwamba ninapiga vita ushirika. Sasa, siko hivyo, nafikiria ushirika ni kitu cha ajabu sana, lakini utaratibu wa ushirika wenu unapoharibika / kuozeana hilo ndilo nililo kinyume nacho. Unaona? Na haijalishi ni wa umoja au wa utatu, au chochote kiwacho, utaratibu ambao unafika mahali ambapo, sasa unasema sisi ni kusanyiko la Mungu (Assemblies of God) [2]

Nenda nyuma, tafuta mahali ilipoanzia. Hebu twende nyuma kule mwanzoni mwa ile picha. Sasa kama hakuna dhehebu katika Biblia, hapo sasa inabidi madhehebu yawe yana mwanzo. Ilianza na kanisa la kikatoliki. Waprotestant wamefanya kutokea katika hilo. [3]

Watu wengi wameshindwa kunielewa mimi ninapozungumzia kuta za kidhehebu. Siyo kwa hilo dhehebu ni kosa, lakini kule kujenga kuta kulizunguka kuwa hakuna mwingine anayeweza kuwa na ushirika, hapo ndipo ile sehemu mbaya ilipo……… Kile kitu, tunapokwenda kufikiri “sisi ndio kundi pekee”. Mungu anaruka juu hapa na kumbariki mtu mwingine na kuonyesha kuwa sisi siyo kundi pekee. Hivyo ndivyo Mungu atendavyo. [4]

Kuna kanisa moja tuu, na hilo siyo dhehebu. Huwezi kulimiliki Kanisa la Mungu. Kuna Kanisa moja tuu na mwili mmoja. Huo mwili ni mwili wa siri wa Bwana Yesu Kristo hapa duniani na kwa Roho mmoja tunabatizwa ndani ya mwili huo. (Ikor. 12:12-27).

Haijalishi lile dhehebu la mtu nilipi, kama anategemea hilo Kanisa lake kwa ajili ya ukombozi, amepotea. Kama mkatoliki anagemea Kanisa katoliki kumuokoa yeye, amepotea. Kama mbaptist anagemea kanisa lake la kibaptisti kumuokoa yeye amepotea. Kama mpentekoste anategemea kanisa la kipentekoste limuokoe yeye, amepotea. Lakini kama hawa watu kibinafsi wanamtegemea Mungu na Yesu Kristo “kwa imani umeokolewa, na siyo kwa matendo lakini kwa neema” (Waefeso 2:8-9) [5]

Kwa hiyo kutakuwa na kuunganika miongoni mwa makanisa na yataungana pamoja, kufanya yale mamlaka ya baraza la makanisa, ambayo tayari wanalo jengo kubwa la U.N (Umoja wa mataifa) na kila dhehebu liko ndani yake. Na inabidi uwe mmoja wa hayo madhehebu vinginevyo utakataliwa. Na huo ndio wakati inabidi tuonyeshe rangi zetu, na kuwa na uhakika kwamba tunaelewa na siyo jambo la kubahatisha, lakini ni kule kujua HII ASEMA BWANA ndipo mahali unaposimamia. Lile Kanisa dogo siku zote limekuwa kwenye uchache, ni kikundi kidogo kama kamba ndogo, kama kauzi kadogo kekundu ambako kanapitia katika Biblia. Lakini siku zote ni kanisa. Na tunapenda kukumbuka hilo. (Luka 12:32, Matayo 7:13-14) [6]

Mungu kamwe hakumbariki Abraham kikamilifu mpaka alipomtii Mungu kikamilifu na kajitenga mwenyewe (na Loti). Na Mungu hata mbariki mtu binafsi au Kanisa, au kusanyiko au dhehebu mpaka kwanza limejisalimisha kikamilifu katika kumtii Mungu.

Dhehebu litakuwa sahihi kama litatoka kama hivi: “Tunaamini juu ya hili koma”, lakini unapoandikisha ushirika na kusema “Tunaamini hili, wakati. Uje katika hili au usije kabisa.

Kama unalisoma hilo, “Ninaamini hili, jumlisha kile Mungu atakachonionyesha mimi, hapo sasa hilo ni sawa. Hiyo ni sawa. “Tunaamini hili, jumlisha chochote tuwezacho kuona katika mapenzi ya Mungu hilo ni zuri”, unaona lakini unaliishia hilo “Tunaamini hili”,.

Kulitokea nini kwa luther mara tuu luther alipoona ile nguzo ya moto? Nini, aliifuata hiyo. Lakini alifanya nini?. Baada ya siku za luther, wakaunda dhehebu wakaliita Lutherani. Halafu lilikufa hapo hapo katika dhehebu, kwa sababu ni kama tuu lile Kanisa Katoliki.

Halafu, jambo la kwanza unajua, baadaye akaja Wasley. Ile nguzo ya Moto iliendelea ikatoka katika hilo dhehebu na ikaendelea mbele. Wasley akaiona, naye akaifuata hiyo. Na mata tuu lile kundi la kwanza walipokuja, wakaunda dhehebu, wakaliita la Wesley Methodist au Kanisa la Kimethodist pale walipounda dhehebu likafa hapo hapo.

Halafu Wapentekoste wakaliona hilo la kutoka, siyo kutoka kuhesabiwa haki, chini ya luther, na utakaso chini ya Wesley, lakini waliona ubatizo wa Roho Mtakatifu, kurudia ile Baraka ya mwanzo. Hao hapo wakaliendea hilo. (Oh jamani), wakaendelea na kuanza kunena kwa lugha na nguvu za Mungu zikitenda kazi kupitia wao. Lakini walifanya nini? Waliunda madhehebu. Na likafa hapo hapo. Lakini sasa ile nguzo ya Moto inatoka imeanza kutembea tena. [7]

Sasa, ninaomba, Mungu, kama nionavyo siku ambayo madhehebu yana mbana mwaminio, na kuwatenga wao, kwa kusema kuwa majina yao lazima yawe katika vitabu vyao, au sivyo wamepotea, hawana uhusiano na kundi linguine. Ni ule mkono laini wa Jehova, ukiwaongoza wao kwenda kwenye Mti wa Uzima.

Namuomba, Mungu, kuwa kila mmoja……….. ninajua watakubali kwa sababu ni Neno lako, na haliwezi kushindwa. Na hebu tuongozwe kwenye Mti wa Uzima, kwamba tuwe wamiliki wa uzima wa milele, unaona mkono wa Mungu, na kwa macho ya Imani, unaangalia kuvuka vivuli hivi ambavyo tunatembea kati yake leo, unaona nchi ya ahadi ikiwa iko mbele yetu. [8]

Tazama hapa, ukichukuwa mbegu nzuri kubwa ya mahindi ambayo ni chotara na uichukue hiyo mbegu, ni mbegu nzuri ya mahindi. Halafu uipande, utapata nini? Kammea kadogo katachipua halafu kanakuwa njano, na kana nyauka. Hivyo ndivyo ilivyo kwa kila dhehebu lilivyo linapokuwa chotara pale maneno ya watu yanapochanganyika na Neno la Mungu. Itafikia mahali pa ishara na maajabu na Yesu alisemaje kuhusu kuamini Neno, hapo itabadilika na kuwa njano na kusema, “hatuwezi kukubali hilo” na hapo linasinyaa tena.

Sikiliza kwa karibu sasa. Nataka ninyi msishindwe kulipata hili. Hakuna kanisa lingine, hakuna ishara, hakuna ushirika mwingine, hakuna serikali nyingine, hakuna ushuhuda mwingine, hakuna kanuni nyingine, hakuna dhehebu lolote linalokubalika nje ya hili. Mungu hakubali kitu kingine chochote ila hiki. “Kristo ndani yako, tumaini la utukufu”. (wakolosai 1:27), kitu pekee ambacho Mungu anatambua.

Hakuna ushirika, hakuna kanisa, hakuna kanuni, hakuna dhehebu, hakuna chochote, kitu kingine chochote kimekufa. Ni vipande pande ambavyo inabidi vikatwe na kuondolewa. Viondolewe kutoka humo ili Kristo aweze kuishi akiwa amechukuwa nafasi ya kwanza ndani yako. (wakolasai 1:18). [9]

Lakini ili mradi Kristo yuko pale, na Roho Mtakatifu anabariki watu, hatujali rangi, kanuni au chochote kile, sisi wote tuko kwenye bwawa moja kubwa la Damu, Baraka za Mungu, kuwa tuu na ushirika chini ya damu ya Yesu Kristo, na hatulioni hilo. Lakini tunapo anza kufikiria, “Unajua dhehebu langu ni nafuu zaidi kuliko la kwao, ni kubwa kidogo kuliko lao. Tunao na watu wengi.” Hapo ndipo shida inapo anza kuingia.

Kwa hiyo wanaanza kulipata hilo, na wanamsahau yeye kuwa yupo pale wakizungumza sana juu yake, bila kumtambua yeye kuwa yu pamoja nao (Luka 24:13-35). Ninatamani ningekuwa na njia ya kuligongomelea msumari.

Tazama, Wale wanafunzi walikuwa wanazungumza juu yake lakini wamesahau ya kwamba alikuwa amelala ndani ya meli hiyo hiyo waliyokuwa ndani yake (Matayo 8:23-27). Na leo hilo ndilo linalotokea makanisani. Tunazungumza juu yake. Tunayo mambo mengi ya kiakili, mpaka watu wamefundishwa katika maandiko mpaka wanaweza kuleta ujumbe ambao huwezi kuunyooshea kidole huo. Lkaini yuko wapi Mungu?. Hilo ndilo nitakalo kujua. Uko wapi ule udhihirisho? Unaona? Mahubiri ya kiakili…………. [10]

Tunasikia mengi juu ya mfumo huu mpya ambao utaleta mifumo ya kidini, unajua, inataraji kuleta amani juu ya dunia, wakati wakatoli na waprotestant wote watakapo ungana pamoja. Wengine huamini uponyaji

wa kiunga, wengine hawaamini, wengine wanaamini hiki na wengine wanaamini kile. Na inabidi ukubali kuacha ile mizozo ambayo walikuwa hawakubaliani wakati wote, uaminio wa injili, ili uingie kwenye lile baraza la Makanisa duniani. Na kila dhehebu inabidi lije pale. Sasa kama madhehebu yamelaaniwa, na kule kuwa katika hilo, inafanya nini? Inakurudisha tena nyuma kule kama Roma ni mama wa madhehebu (ufunuo 17:1-6). Naye ni Yule mnyama na ile chapa ya mnyama (Ufunuo 13:16-18). Halafu wakatengeneza sanamu kwa mnyama Yule, baraza la makanisa yote yana tengeneza ile chapa kwa mnyama (ufunuo 13:11-15). Kwa hiyo ni moja kwa moja tena unarudi kwa ile alama ya mnyama. Mfumo wa dunia, madhehebu, yameleta mfumo ambao utaileta ile picha ya mnyama. [11]

Sasa tunaweza kuona kwa mifano ya Agano la kale pale mahali alipochagua kuliweka jina lake na wapi sasa…….. Na sasa kama vile kivuli kilipita sakafuni. Nikasema, hicho ni kivuli, kikiwa ni mfano, kwa hiyo , waabuduo wanaweza kuona kile kivuli cha Agano la kale kikipotea na kuja kwenye uhalisia wa Agano jipya (Waebrania 10:1).

Sasa zile karamu zote, zile sikukuu, ile maskani, zile mbao (miti), kila kitu katika ile maskani, kila kitu kilikuwa kina mueleza Kristo. Matokeo yote, sheria zote, kila kitu kilikuwa mfano wa Kristo. Tumepitia hayo kila wakati tukiyarudia rudia hapa katika maskani. Halafu tunaona kwa hayo kuwa kila kanuni, kanisa, na dhehebu linaachwa mbali kule nyuma. Haliko kabisa hata kwenye mashindano kabisa. Kila kanuni, kila kanisa, kila dhehebu limeachwa kabisa nje. Hakuna mahali kwa ajili yake hata kidogo. [12]

Sasa, ninaamini kuwa Yesu Kristo anashika kila Neno lake. Maandiko yote yamevuviwa. Naamini hatunayo haki hata moja, na tutahukumiwa kwa hilo, kama tutaongeza Neno moja au kuondoa Neno moja katika hilo Ufunuo 22:18-19 inasema hivyo. Naamini Yeye ni Yule jana leo na hata milele.

Kwa hakika nawaheshimu Walutheri kwa msimamo wao katika siku yao. Wamethodisti kwa utakaso katika siku yao, na Wapentekoste katika msimamo wao katika siku yao. Lakini tunaishi katika siku nyingine. Tunaishi wakati kulipokuwa na ubua, mauwa, kapi ambalo lilifanana sana na ngano, lakini ngano iko ndani ya kapi. Lile kapi lilikuwa likiishikilia ngano. Likizuia jua lisiichome hiyo. Na sasa lile dhehebu linajitoa mbali na ngano, ili ikae katika uwepo wa jua ili ikomae. Hakutakuwa na vyama vyovyote vitakavyo inuka. Haiwezekani. Huu ni mwisho wa hilo. Tumekuwa mara nyingi na uamsho ambao uliweza kuchukuwa miaka mitatu, ujumbe unapoanza, wanaunda mashirika ya huo.

Hili limekuwepo kwa zaidi ya miaka ishirini na hakuna chama chochote na hakiwezi kuwa. tuko katika wakati wa ngano, wakati wa mavuno. Ninaweza kusihi ili mashine ya kuvunia inakuja siku moja tunaenda nyumbani, m oja ya siku hizi. Hiyo ni kweli “Yeye ni yule jana leo na hata milele” (Waebrania 13:8). [13]

Ona sasa ni nani kiongozi wa dini hii ya kisasa ya wakati mwovu? Ni shetani akichukua mti wa mema na mabaya na kuuweka nje pale (Mwanzo 3:1-7, 2:15-17), akilileta kanisa lake la kupendeza la bibi arusi kwenye baraza la makanisa kwa ajili ya ile ndoa (au arusi) kanisa lake lakupendeza la kisayansi likiwa na digrii zote ziwe za kupatikana PhD’S kutoka ndani ya kanisa la Kristo, zile Ph D’S, nje ya Wabaptist, Presbyterian, wapentekoste na wote aliwaleta na mapambo yao yapendezayo, na makanisa makubwa, baraza lote la ekumenia, “walisema tu mmoja”. Kamwe hiyo wao hawatasamehewa kuvaa nembo ya dhehebu ni ile chapa ya mnyama. Tumeshaipitia hiyo juu ya kulifanya hilo. Kimbieni watoto, kimbieni. Mnaona? Kanisa kuu la kupendeza kwenda arusini Ekumeni, kuvaa chapa yake! Kaptura (hakika) mavazi ya kidunia, ya kizinzi, rangi, wanafunzi wazuri wa shetani kuwanasa wana wa Mungu……… kuolewa na kijana aliyezaliwa kikamilifu na kundi hili lililopotoka kama hilo. Hiyo ni sahihi. [14]

Kila mara kuna mapacha na hiyo ndiyo sababu……….. usisahau hili, kundi dogo. Kanisa katika siku za mwisho litaenda kuwa mapacha, karibu sana kiasi cha kuweza kumdanganya mteule. Matayo 24:24. Unaona? Ni uamsho wa kipentekoste, unaonekana kuwa kama kile kitu halisi, mpaka inaweza kumdanganya yule mteule kama ingewezekana. Na baadae kidogo kama nitapata nafasi. Nataka niwaelezee vile, ule uteule unavyokuja, unaona. Hilo litaenda kuwadanganya wao, kwa sababu linaonekana kama ni jambo lile lile. Unaona, ni baba wawili tuu, ndivyo hivyo tuu mama yule yule, kanisa lile lile, kikundi kile kile, kitu kilekile. Mahali mbegu inapotua ni pale pale, ambapo Neno linaangukia lakini mmoja wao, kama hapa, pamepotoka. Unaelewa?. Unaona moja wapo ni upotovu, kwa sababu ni Baba asiye sahihi. Unawaongoza watu kuunda vyama badala ya Neno la Mungu. Na kila kitu ni mapacha katika vita vya maisha haya. [15]

Subiri mpaka usikie “Ule mkondo wa nyoka” (Trail of the Serpent) vema sasa wao wanafikiria dhehebu lao ndilo linalo sajili pamoja na Mungu. Mungu hatakusikia wewe mpaka wewe uwe mmethodist au mbaptisti au uwe wa utatu au uwe wa umoja au kitu fulani kama hicho. Hiyo siyo sahihi.

Lakini kumbuka katika hayo yote, kama kuna kitu fulani katika moyo wa mtu au moyo wa mwanamke ambaye anaamini kuwa hilo ni sahihi, hapo sasa lazima kuwe na mahali fulani ambapo ni sahihi. Kama nilivyosema mara nyingi, “Kilindi kikiita kilindi, kuna kilindi cha kuitikia huo mwito. (Zaburi 42:7).

Mungu siyo mwanzilishi wa madhehebu, kwa sababu madhehebu ni babiloni, na Yeye siye mwanzilishi wa machafuko. Huhitaji kuwa wa kiakili sana kuliona hilo. Hiyo ni Babiloni. [16]

Yesu alisema kuwa Yeye akiondoka Atampeleka Roho Mtakatifu (Yohana 14:15-18). Ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea. Hiyo ni sawa. Dunia au utaratibu wa dunia hauwezi kumpokea yeye. Hivyo ndivyo madhehebu yalivyo ni taratibu za dunia. Nionyeshe mimi utaratibu wa kanisa la kidunia ambalo limejazwa na Roho Mtakatifu. Napenda kuliona hilo. Kama unaweza kunionyesha mimi hilo kanisa utakuwa unalitoa makosa Neno la Mungu. Hapana bwana. Hakuna hata mmoja wa hawa wajumbe aliyekuwa na utaratibu wa kidhehebu. Wakitolewa nje au walitoka nje kwa sababu walikuwa wamechoshwa na dhambi ya (ushirika) madhehebu. Itawezekanaje Roho Mtakatifu awe katika dhehebu (ushirika) wakati ni (ushirika) ndio unao chukuwa nafasi ya Roho Mtakatifu na dhehebu linachukuwa nafasi ya Neno? Kumbuka, ushirika wa kidhehebu ni “Kifo”. Haiwezi ikawa vinginevyo kama dunia ina chukua mamlaka, Roho anaondoka. [17]

Sasa huwezi kuchanganya kanuni za dhehebu pamoja na Neno, kwa sababu vimepingana sana. Kimoja kwa kingine. Hivyo ndivyo shetani alivyojaribu kufanya na akili zake kwa uelewa wa kiakili kwa Hawa. Alikubali kuwa Mungu amesema hivyo. “Na akasema hakika hutakufa” (Mwanzo 3:1-7) unaona, wao waliliamini hilo na ndilo ambalo kanuni / maungano yamefanya usiku wa leo. Madhehebu yamewatenganisha watu na Neno la Mungu. Yesu alipokuja alisema, “Ninyi kwa kanuni zenu mmelifanya Neno la Mungu lisiwe na nguvu kwa watu” (Marko 7:6-9). Na kupitia kanuni zetu tumeleta mfarakano wa ushirika na Roho Mtakatifu kulipaka mafuta Neno la Mungu ambalo limetengwa kwa wakati. Tumewatenganisha watu na madhehebu kiasi kwamba hawana nafasi ya kuweza kuliona Neno. [18]

Kumbuka Israel, walitembea mchana na usiku na nguzo ile ya moto. Ile nguzo ya Moto ilipotembea, walitembea pamoja nayo. Na kumbuka ilikuwa moto wakati wa usiku na wingu wakati wa mchana. Kwa hiyo inaweza kuja mchana au usiku, wakati wowote. Lakini vyovyote iwavyo, kulikuwa na utambulisho uliofanyika, kwamba wasishindwe kuiona. Ilikuwa ni Nuru usiku na Wingu wakati wa mchana nao waliifuata hiyo. Ndiyo Bwana. Jambo lile lile (Kutoka 13:21-22, 14:24).

Martin Luter aliiona, Alifanya nini? Alitoka kutoka kwenye ukatoliki, lakini walifanya nini? Walijijengea ukuta mdogo kuwazunguka na kusema sisi ni walutheri. Hili ndilo lenyewe.

Wesley aliiona ikitoka kutoka hapo. Alitoka na yeye, walifanya nini? Walijenga ukuta mdogo kuwazunguka wakisema hili ndilo lenyewe. Ile Nuru ilifanya nini? Ilitoka na kuendelea kutembea.

Wapentekoste wakaiona. Wakafanya nini? Walitoka kutoka kwa wa Wesley na wanazarayo, nakadhalika, wakafanya nini? Wakajenga ukuta mdogo kuwazunguka wakijiita sisi ni wa umoja na sisi ni wa utatu na sisi ni united (walioungana) na mambo hayo yote. Alifanya nini? Mungu alitembea kutoka humo. Unaona, hatuwezi kufanya hivyo, inabidi tufuate kila siku, kila saa ya kila siku. Kila hatua katika njia. Lazima tuongozwe na Bwana Yesu Kristo. Kama hatufanyi hivyo, tunachukuwa maisha ya kidhehebu. Na maisha yasiyo mfuata Kristo kila siku hayamstahili. [19]

**NUKUU ZA KIINGEREZA.**


(1) Kwa nini sisi sio dhehebu (58 – 0927), Aya 15 – 16
(2) Kuelezewa kwa uungu (61 – 0425 B), Uk. 13
(3) Ubatizo wa Roho Mtakatifu (58 – 0928M) Aya 105
(4) Msikieni Yeye (59 – 0424E) Aya E -4
(5) Haikuwa hivyo tangu mwanzo (60 – 1127M) Aya E – 26
(6) Maono ya Patimo (60 – 1204E), Aya 57
(7) Jehova Jireh (61 – 0209) Aya E 47 – 48
(8) Kule kutoka kwa tatu ( 63 – 0630M) Aya 57
(9) Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa (63 – 0728) uk 41-69
(10). Nenda kamuamshe Yesu (63 – 1103) Aya E – 41

(11) Dunia inamomonyoka vipande pande (63 – 1127) Aya 157

(12) Mahali Mungu alipochagua pa kuabudia (65 – 0220) Aya 37-38

(13) Je Mungu hubadili nia yake (65 – 0427) Aya 212 – 214

(14) Mungu wa wakati huu mwovu (65 – 0801M) Aya 145

(15) Nguvu ya kubadilisha (65 – 103M) Aya 135 – 136

(16) Mahali pekee Mungu alipotoa pa kuabudia (65 – 1128M) Aya 66-67,92

(17) Wakati wa Kanisa wa Sardi (Nyakati 7 za kanisa – uk – 251)

(18) Muungano usiioonekana wa Bibi Arusi (65 – 1125) Aya 11

(19) Maisha yako yanaistahili Injili ya Kristo (63 – 0630 E) Aya 72-76

---

*jiwe la kiroho la kujengea na 197 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebelievers.de*

---

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.*

*(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa: Charles E. Y. Kanju,*

*Box 5138, Tanga*

*E-mail: chaelika@hotmail.com*

*Cell.phone 0784704299*